*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1), 136-150*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.8

# Ubainishaji wa Mitindo katika Methali za Wamasaaba nchini Uganda

*Wanyenya Willy*[1]

## Ikisiri

Makala hii inafafanua mitindo katika methali za Wamasaaba nchini Uganda. Lengo kuu la makala ni kueleza jinsi methali za Wamasaaba zinavyotumia mitindo mahususi kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Utafiti huu umefanyika uwandani. Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Uelewaji Ujumbe kwa kutumia lugha ya moja kwa moja. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa mitindo katika methali za Wamasaaba inahusiana na: uteuzi wa maneno, idadi ya maneno katika methali, matumizi ya maneno ya kawaida, urejeleaji wa vitu vya kawaida, matumizi ya lugha kisanaa na matumizi ya maelezo katika methali badala ya maswali.

## 1.0 Utangulizi

Lugha ni chombo cha mawasiliano katika jamii. Ujumbe hauwezi kupitishwa bila kutumia lugha. Lugha zina vipengele tofautitofauti. Kuna vipengele vya kifasihi na vya kiisimu. Kwa upande wa fasihi, kuna vipengele kama vile methali, shada, tashbihi, tanakali sauti, istiari, misemo, n.k. Kwa hiyo, vipengele hivi vinastahili kutafitiwa ili kukuza lugha za asili ambazo kwa watu wengi zinaonekana kuwa duni. Kutokana na jambo hili, makala hii imejikita katika utanzu wa methali. Makala inaeleza mitindo katika methali za Wamasaaba nchini Uganda. Kila jamii ina methali zake zinazoweza kutofautiana au kufanana na za makabila mengine. Kwa hiyo, makala hii inaangazia methali za Wamasaaba peke yake. Zile za makabila mengine hazijaguswa.Kulingana na makala hii, *Kimasaaba* ni lugha ambayo haijatiliwa maanani na wenyeji. Watu ambao wanapaswa kuiendeleza wanaipuuza. Kufikia mwaka 2019, lugha hii haikuwa ikifundishwa shuleni wala katika vyuo vikuu na haikuandikiwa vitabu. Waliofanya utafiti waligusia vipengele vyake lakini katika fasihi ya Kiingereza au lugha zingine za kigeni. Wao hawakuhusika moja kwa moja na lugha hii. Kwa mfano, wanafunzi katika vyuo vikuu walikuwa wakifanya tafiti zao kuhusu mada mbalimbali za lugha hii katika

[1] Mhadhiri, Shule Kuu ya Kibiashara ya Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda. Baruapepe: willywanyenya@gmail.com

fasihi ya Kiingereza. Hali hii ilifanya Kimasaaba kubaki nyuma. Kwa hiyo, makala hii inaeleza mitindo katika methali za Wamasaaba. Methali kama mojawapo ya misingi ya lugha ni sanaa ambayo inatumiwa na watu waliobobea katika utumiaji wa lugha husika. Siyo kila mtu ana uwezo wa kutumia methali katika mazungumzo ya kila siku. Ni watu wachache ambao wana uwezo wa kufanya hivyo. Sanaa hii imeathiriwa pakubwa sana na jinsi Wamasaaba wengi, hasa vijana, wanavyoipuuza lugha mama yao. Wazee ambao wamebobea katika matumizi ya methali wanapokufa, methali pia zinakufa. Hii ni kwa sababu methali zao hazijaandikwa popote. Shuleni na vyuoni, wanafunzi hung'ang'ana na ujifunzaji wa methali za Kiingereza na lugha zingine za kigeni. Mambo haya yameshughulikiwa katika makala hii.

## 2.0 Taarifa za Kimsingi Kuhusu Mitindo

Daniel (2017) anaeleza kuwa mtindo katika lugha hurejelea jinsi watu wanavyozungumza au wanavyoandika kwa kuzingatia mambo yanayowasababisha kufanya hivyo. Danielanasema kuwa kuna mitindo mingi ya lugha. Anadai kwamba mifano ya mitindo inaweza kupatikana kwenye barua. Kulingana naDenis, katika barua rasmi, anayeandika huanza kwa maneno kama: *Dear Sir/Madam* au *Dear Mr. X* na kuishia kwa maneno kama: *Yours faithfully* au *Yours sincerely*. Na katika barua zisizo rasmi, anayeandika anaweza kuanza kwa maneno kama: *Hi* au *Dear X* na kuishia kwa maneno kama *Love,* n.k.

Kwa mujibu wa Daniel (2017), kuna mitindo kadhaa inayotumiwa katika mazungumzo. Anasisitiza kuwa mitindo hiyo inaweza kubainika kisintaksia, kimsamiati, toni, n.k. Anafafanua kwamba mitindo hiyo inategemea kiwango cha elimu ya mzungumzaji, hadhi yake kiuchumi, na hali aliyonayo katika maisha. Kwa mfano, mtu huzungumza kwa njia tofauti kama ndiyo amepata kazi bora au kama amefiwa. Katika mazungumzo, kuna kupanda na kushuka kwa sauti. Hivi viwili vinaweza kujitokeza katika hali ya kutisha, kuomba, hasira, furaha, n.k. Mabadiliko katika lugha au lahaja ya lugha huwa yanaleta mitindo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Gunawan na wenzake (2019), mitindo ya lugha hufasiliwa kama uteuzi wa maneno yanayotumiwa na kundi fulani la watu wanapozungumza. Makala hii imejikita katika mazungumzo na kueleza jinsi Wamasaaba wanavyosuka lugha kisanaa kwenye mazungumzo. Makala inaeleza jinsi Wamasaaba wanavyotumia methali wanapozungumza. Makala haijagusa vipengele vingine vya lugha kama vile: tashbihi, shada, tanakali za sauti, n.k. Hii ni kwa sababu lugha ni pana na yafaa kila kipengele husika kitafitiwe kivyake.

## 3.0 Tatizo la Utafiti

Kwa mujibu wa Mulumba (2021), baadhi ya lugha zetu zimeanza kufa polepole kikiwemo *Kimasaaba*. Mulumba anaeleza kuwa kupoteza lugha ni kupoteza

utamaduni, na kupoteza utamaduni ni kupoteza maarifa ya jamii. Anaendelea kusema kuwa ni jambo la kusikitisha kuona kwamba nchini Uganda, watoto kutoka kwenye familia za wazazi wasomi hawazungumzi lugha mama zao. Mwandishi anasema kuwa katika familia hizo, wazazi hawataki kuwasiliana na watoto wao kwa kutumia lugha mama. Mulumba (2021) anaeleza kuwa ni muhimu sana kukuza lugha mama, kuziendeleza na kuzilinda. Anasema mambo haya matatu yanaweza kutekelezwa kwa kuziandika lugha hizo, kuziongea na kuzitafiti. Elunya (2009) pia anasema kuwa Kimasaaba ambacho ni lugha inayozungumzwa na Wamasaaba nchini Uganda imeanza kufa polepole. Anaendelea kusema kwamba lugha hii imeanza kufa kwa sababu wenyeji huwa wanapenda kuzungumza *Kiganda* kuliko lugha yao. Anasema kuwa katika viunga vya Mbale ambao ni mji mkuu wa eneo hilo, watu huwa wanaongea Kiganda badala ya *Kimasaaba*. Anadai kuwa hali hii iliwekewa msingi na Semei Kakunguru, Mganda ambaye alipelekwa na Wazungu kutawala Wamasaaba katika enzi za ukoloni. Hivyo basi, kulingana na maelezo ya wataalamuhawa wawili, kuna mahitaji ya kukuza, kuendeleza na kuilinda lugha hii. Njia mojawapo ya kufanya hivyo ni kuitafiti. Hii ndiyo sababu mtafiti ameamua kuandika makala kuhusu mitindo ya methali. Mtafiti amejikita katika mitindo kwa sababu kipengele hicho hakijashughulikiwa na wasomi ambao wameitafiti lugha hii.

**3.0 Mkabala wa Utafiti**

Ukusanyaji wa data umefanyika uwandani kwa njia ya mahojiano. Watoataarifa walikuwa wazee wa vijijini. Mtafiti aliwachagua wazee kwa sababu wamebobea katika matumizi ya methali. Mtafiti hakutumia watu wa mijini kwa sababu wameathiriwa na lugha za kigeni. Sampuli za wahojiwa zilijumlisha wazee wa kiume 50 na bikizee 50. Kwa ujumla, mchunguzi alikuwa na sampuli ya watoataarifa 100. Mtafiti hakuteua wahojiwa hao kwa kutumia njia maalumu. Aliwahoji kama alivyokutana nao. Mtafiti alitumia mahojiano ili kupata picha halisi ya mambo katika jamii hii. Kazi ya nyanjani ilihusika kwa kiasi kikubwa na ukusanyaji wa methali. Methali zilizotajwa na wahojiwa ziliandikwa kwenye kijitabu. Maelezo kuhusu methali hizo pia yaliandikwa. Mtafiti alifanya hivyo ili jambo lolote lisimpite. Kwa kufanya hivyo, aliweza kuwasilisha data kama alivyozipokea kutoka kwa wahojiwa wake.

**4.0 Maandiko ya Tafiti Mbalimbali**

Utafiti wa Aleta (2021) unaeleza jinsi wanawake wanavyowakilishwa katika methali za Kioromo. Ili aweze kutimiza lengo lake, Aleta (2021) alikusanya methali zenye uhusiano na wanawake katika jamii ya Waoromo. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa wanawake wamewakilishwa kwa uwazi katika methali hizo. Anasema kwamba methali hizo ama zinawainua wanawake au

zinawadunisha. Anadai kwamba methali hizo zinawainua wanawake kwa kuwadhihirisha kuwa ni wazazi wanaoheshimiwa katika jamii. Kwa upande mwingine, methali hizo zinawadunisha wanawake kwa kuwadhalilisha kama vile kuangaliwa kama viumbe dhaifu na wasiojua lolote. Kwa kutazama maelezo haya, inabainika wazi kuwa Aleta (2021) ameeleza jinsi methali zinavyowasilisha ujumbe kwa jamii. Hata hivyo, hajaeleza mitindo inayotumiwa katika kuwasilisha ujumbe husika. Hivyo basi, jambo hili linaacha mwanya ambao utafiti huu umeuziba kwa kutoa maelezo kuhusu mitindo ya methali.

Kulingana na Bukenya na wenzake (2008), fasihi simulizi inatusaidia kujijua sisi wenyewe, binadamu wenzetu, mazingira yetu na historia yetu. Wataalamu hawa wanaendelea kusema kuwa hadithi, nyimbo, methali, vitendawili na mizaha, katika fasihi simulizi hutumia maneno mahususi pamoja na sura kuwaelezea binadamu, hisia zao na tabia miongoni mwao. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, utendaji hudhihirisha matukio yanayotokea maishani mwetu na katika historia ya jamii zetu. Wanasema kuwa fasihi simulizi hutupa picha za watu, vitu na matukio kama vile ndoa, maombolezo, n.k. Wametaja tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Kila mojawapo ya tanzu hizo inastahili kufanyiwa utafiti wa kina. Kwa hiyo, miongoni mwa tanzu zote ambazo zimetajwa, makala hii imejikita katika utanzu wa methali.

Castagna (2022) ameshughulikia methali za Kijibbali na anasema kuwa kwa karne nyingi, wazungumzaji wa lugha hii wamekuwa wakipitisha maarifa yao kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kutumia mdomo. Kulingana na Castagna, lugha ya Kijabbali haikuwa ikiaandikwa. Watu walikuwa wakipitisha ujumbe kwa njia ya mazungumzo. Anadai kuwa amekusanya methali 210 na kuzifasiri katika lugha za Kiarabu na Kiingereza. Hata hivyo, anaeleza kuwa tafsiri hizo zinapotosha. Jambo hili linaonesha kuwa mwandishi hajashughulikia mitindo katika methali. Ameshughulika tu na ukusanyaji wa methali na kuzifasiri katika lugha zingine. Jambo hili linaonesha kuwa kuna mahitaji ya kuchunguza mitindo ya methali katika lugha tofautitofauti.

Kwa mujibu wa Finnegan (1976), mwingiliano wa methali na mitindo mingine ya lugha umeleta utata wa kutofautisha methali na semi zingine. Kwa mfano, siyo rahisi kutofautisha methali na misemo. Kwake, kazi nyingi za methali ambazo zimechapishwa hupuuza jambo hili. Kulingana na Finnegan, methali nyingi za Wanyembezi na Wadoke zina utata huu. Finnegan anasema kwamba, fasili halisi ya methali ni jambo ambalo si rahisi. Hata hivyo, anasema kwamba, kuna makubaliano ya jumla kuhusu elementi zinazounda methali. Kwa mfano, methali huwa fupi na zina maana kubwa ndani yake. Mara nyingi methali huwa na maana fiche kwa njia moja au nyingine. Kwa kuzingatia maoni ya Finnegan (1976), kuna mahitaji ya wasomi kushughulika na utafiti wa methali. Hii ni kwa

sababu ya utata unaoizunguka dhana ya methali. Kutokana na mtazamo huu, makala hii imeeeleza mitindo ya methali za Wamasaaba.

Mieder (2016) anaona kuwa methali huwa sentensi fupi inayojulikana na yenye maarifa, ukweli, tabia, na maoni ya kiutamaduni yanayojitokeza kistiari ambayo inarithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mtaalamu huyu pia anajaribu kueleza maana ya neno ‘methali.’ Ni wazi kuwa hajajishughulisha na mambo mengine kama vile miundo ya methali na matumizi ya lugha, jambo ambalo limeshughulikiwa katika makala hii.

Norrick (2010) amechora jedwali lenye mambo maalumu ili kutofautisha methali na semi zingine kama vile misemo na mizaha. Jambo hili linaonesha kuwa mtaalamu huyu alijikita katika kueleza tofauti zilizopo baina ya methali na semi zingine. Mambo mengine kama vile matumizi ya lugha na mitindo hayakuwa miongoni mwa mambo aliyoyatafiti. Kwa hiyo, jambo hilo linaacha mwanya ambao umezibwa katika makala hii. Hii ni kwa sababu makala hiie imeeaeleza matumizi ya lugha katika methali za Wamasaaba nchini Uganda.

Kwa mujibu wa Mbusya na Chomba (2018), methali huwa na miundo tofautitofauti. Wanasema kuna methali ambazo zimeundwa kwa kutumia maswali ya balagha. Kwa mfano, kamba haikuwa kamba, itakuwa kambaa? Pia, wanadai kwamba utafiti kuhusu methali umefanywa na watafiti mbalimbali ambao wameshughulikia taaluma hii ambayo ni pana na changamani. Wanaeleza kuwa kadiri watafiti wanavyozidi kushughulika na kazi yao ya utafiti, ndivyo wanavyozidi kufichua maarifa muhimu na kuyatumia katika nyanja za masomo ya juu ulimwenguni. Maelezo ya wataalamu hawa yamechangia makala hii kwa njia kuu tatu. Kwanza, ni aina ya mada iliyotafitiwa, yaani ukinzani wa methali. Mada hii inaonesha kuwa kuna mambo mengi sana kuhusu methali ambayo yanaweza kutafitiwa. Ingawa mchunguzi hajaendeleza utafiti wake kuhusu ukinzani wa methali, mada hii imempa fikra tambuzi ambazo zilimsaidia kuibuka na mada ya mtindo ambayo imeshughulikiwa katika makala hii. Hivyo basi, mada hiyo ilikuwa kama kichochezi chakuanzisha utafiti huu. Pili, kauli ya wataalamu hawa kuwa kipera cha methali hakijatafitiwa vya kutosha, ilimchochea mtafiti kufanya uchunguzi wake. Hii ni kwa sababu, usemi wenyewe unakaa kama kaulimbiu ukiwataka wasomi watekeleze tafiti madhubuti kuhusu methali. Tatu, ni kauli ya watafiti hawa kwamba methali huwa na miundo tofautitofauti. Kauli hii inamaanisha kuwa kuna mahitaji ya kutafiti miundo ya methali katika lugha mbalimbali. Kauli hizi tatu zilimpelekea mchunguzi kuuendeleza utafiti huu.

Ogden (2022) amefanya utafiti wake kuhusu methali kwa kuzingatia dhima ya methali hizo kwa jamii. Anasema kuwa methali ni kipengele muhimu sana katika fasihi simulizi na kimekuwa kikichunguzwa na wasomi wengi. Anaeleza kuwa, juhudi za kuchunguza methali zilifanywa sana kati ya 2011-2020. Anadai kuwa watu mbalimbali walikuwa wakichunguza vipengele tofauti katika methali

kama vile muundo, sifa, maadili, adhabu na uchumi. Maelezo haya kuhusu methali ni finyu sana. Mtafiti hajatoa maelezo kuhusu mitindo ya methali inayotumiwa katika kuwasilisha ujumbe. Hivyo basi, jambo hili linaacha mwanya ambao umezibwa katika utafiti huu.

Kulingana na Omobola (2014), ustaarabu umeathiri pakubwa sana vizazi vya sasa. Jamii zimeathiriwa ama vizuri au vibaya kutokana na ustaarabu. Omobola anasema kuwa hakuna sehemu ya maisha ya binadamu ambayo haijaguswa hasa na utamaduni ambao ni kipengele muhimu sana, kikihusisha mambo kama vile maadili, imani au hata lugha ambayo inatofautisha makabila mbalimbali. Msomi huyu anasema kwamba kutokana na ustaarabu, mambo mengi ya kiutamaduni yameanza kutoweka katika jamii au yamo hatarini. Anaendelea kusema kuwa kinachohuzunisha zaidi ni kuona lugha zetu zikiathiriwa kwa kasi sana. Lugha mama zetu hasa barani Afrika zimeanza kutoweka huku lugha za kigeni zikichukua nafasi. Maelezo haya yanaonesha kuwa kuna mahitaji ya kuzitafiti na kuziendeleza lugha mama zetu . Aidha,ni jambo hili ndilo lililomsukuma mtafiti kuendeleza utafiti huu ili achangie katika kuhifadhi lugha mama.

Samadi (2022) ameshughulikia umuhimu na manufaa ya methali katika kusoma na kujifunza lugha. Amejikita hasa katika athari na manufaa ya methali katika kuendeleza sarufi, msamiati na stadi za lugha za wanafunzi. Ni kweli kwamba msomi huyu ametaja jambo la methali, hata hivyo, hajaeleza jinsi methali zinavyotumiwa kutimiza mambo hayo. Kwa mfano, angeeleza mitindo inayotumiwa katika kuendeleza sarufi, msamiati na stadi za lugha, jambo ambalo hajalifanya. Ni jambo hili ndilo lililomsababisha mtafiti kuendeleza utafiti huu kwa kutafiti mitindo ya uwasilishaji katika methali za Kimasaaba nchini Uganda.

Wamitila (2003) alishughulikia fasihi simulizi kwa ujumla na akasema kwamba, dhima mojawapo ya fasihi simulizi ni ile ya kuburudisha. Wamitila anafafanua kuwa fasihi simulizi huwa inatumika kwa ajili ya kuburudisha. Kwa mtazamo wake, tanzu za fasihi simulizi kwa mfano, masimulizi ya kinathari, mashairi, methali na vitendawili hutumiwa katika kuburudisha hadhira. Anasisitiza kuwa, ni jambo la kawaida kuona vijana au watoto wakitegeana vitendawili kama kiburudisho. Kwa kuzingatia maoni yake, hadithi fupi, ngano na visasili pia huwa na lengo la kuburudisha. Maelezo haya yanaonesha kuwa mtaalamu huyu ameshughulika na tanzu za fasihi simulizi kwa jumla. Kwa hiyo, kila mojawapo ya tanzu hizo inafaa kutafitiwa na kubainisha vipengele vilivyopo. Kwa kuzingatia wazo hili, makala hii inaeleza mitindo katika methali za Wamasaaba.

## 5.0 Msingi wa Nadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Uelewaji Ujumbe kwa kutumia lugha yenye maana fiche. Mwasisi wa nadharia hii ni Reem (2022). Kulingana na

nadharia hii, wazungumzaji wenyeji hunatumia tashbihi, istiara, tanakali sauti, shada na vipengele vingine vya lugha. Kwa mujibu wa Reem (2022), matumizi ya vipengele hivyo hufanya wenyeji waelewane bila matatizo yoyote. Hata hivyo, anasema matumizi yake hufanya mambo kuwa magumu kwa wageni wanaojifunza lugha husika. Kulingana na maelezo ya Reem (2022), tafiti nyingi zimedhihirisha ugumu unaotokana na matumizi ya lugha yenye maana fiche kwa wageni wanaojifunza lugha husika. Nadharia hii imekuwa muhimu sana katika utafiti huu kwa sababu ilimwelekeza mtafiti katika kuchunguza jinsi wazungumzaji wa Kimasaaba wanavyobuni maneno yanayounda methali zao na namna wanavyoyapanga maneno hayo na kujenga taswira kwa wasikilizaji. Kwa kuzingatia nadharia hii, mtafiti amechunguza uwasilishaji ujumbe kwa kutumia maneno machache, matumizi ya maneno teule, toni za uwasilishaji, idadi ya maneno katika methali, matumizi ya lugha kisanaa, miundo ya methali zinazoruhusu na zisizoruhusu majibu, na kutumia maelezo badala ya maswali. Mambo haya ndiyo yalikuwa kiini cha utafiti.

## 6.0 Uchanganuzi wa Methali za Wamasaaba Kwa Kuzingatia Hoja Tofauti

### 6.1 Ushauri

Kwa kawaida, methali huwa zinatoa ushauri kwa wasikilizaji.Katika, Kimasaaba pia jambo hili linatekelezwa. Tazama mifano ya methali na uchambuzi unaofanywa:

*Umumasala alankyilama wamulondakho*. Tafsiri yake katika Kiswahili ni kuwa: "Mama mkwe hawezi kutangulia ukamfuata." Hii inamaanisha kwamba mtu akimfuata mzazi wa kike wa mkewe, anaweza kupendezwa na maumbile yake akamtamani. Jambo hili ni mwiko katika jamii, kwa sababu linaweza kumsabaabisha mkwe kumtongoza mama mkwe wake.

*Umumi aamba esi ola* (mtu mfupi hushika pale ambapo mkono wake unaweza kufika). Maana ya methali hii ni - si vizuri kung'ang'ania mambo makubwa. Mtu anastahili kufanya kile anachokiweza. Kama ni kuahidi pesa kwenye michango, aahidi kile atakachoweza kutoa. Hii ni kwa sababu watu wengine wakiona wenzao wanaahidi pesa nyingi, wao hufanya hivyo pia, halafu baadaye wanashindwa kutekeleza kile walichoahidi. Kwa hiyo, Wamasaaba hutumia methali hii kushauri watu wasiwe wanaahidi vitu ambavyo hawawezi kutekeleza.

*Bunuku bulyama lutwela* (cheche za ngono haziji mara moja). Ujumbe hapa ni, ukiwa na mahitaji ya msaada ukasaidiwa, ni lazima utahitaji msaada mara nyingine kama ilivyo na cheche za ngono. Usemi huu hutumiwa kushauri watu hasa wale wanaokopa pesa kisha wanakataa kulipa. Katika jamii zetu, kuna watu ambao wakikopeshwa hela, hawataki kulipa. Kwa hiyo, waliotoa pesa huwa wanatumia maneno haya kuonya wahusika.

*Bulebe indekhelo.* (Chakula ndicho kinaonesha kuwa fulani ni jamaa yako). Kulingana na sentensi hii, ukitembelewa na mwanaukoo, unastahili kumpa chakula (ukarimu). Methali hii hutumiwa kwa sababu kuna baadhi ya watu ambao hawajali wageni. Mgeni anafika nyumbani, wanamwangalia tu mpaka anapoondoka. Kiutamaduni, mgeni hawezi kufika kwa jamaa yake halafu akaondoka bila kula.

*Shifiti shibonekha wangu.* (Kitu kidogo hupatikana haraka). Kinachowasilishwa hapa ni, si vizuri mtu kuomba kitu kwa wingi. Kama ilivyo kawaida, kuna watu ambao wanataka wapewe kwa wingi kitu wanachoomba. Funzo kwao ni, wakitaka usaidizi, waombe kitu kidogo. Wakitaka kiasi kikubwa, basi, waende dukani wakanunue.

*Shisili inga shafunikhile kumwini usomo kukundi.* (Jembe likivunjika mpini, unatia mwingine). Kauli hii ina ushauri ambao ni, mtoto akifariki, mwanamume hastahili kujinyonga bali ashughulike na kumpa mkewe mimba nyingine. Mawaidha haya yanalenga wanaume wanaojaribu kujiua baada ya kupoteza watoto wao, yaani yanawahimiza wazazi wawe wavumilivu wanapofiwa.

*Uwukhalilikha alya kalobile* (Mvumilivu hula mbivu). Kinachoelezwa ni, si vizuri kuwa na haraka. Maelezo haya hutumika kwa ajili ya kushauri wale binadamu ambao si wavumilivu. Kuna watu ambao hawawezi kuvumilia. Kwa mfano, chakula hakijaiva, wanataka kipakuliwe au matunda hayajaiva vizuri, wanataka kuanza kuyala. Kwa hiyo, methali hii hutumika kuwashauri watu kama hao kuwa na subira. Mfano ni, endapo mtu ameahidiwa kitu yafaa awe na matumaini akijua ahadi itatekelezwa.

*Bubutsutsukha ukhwayama bwosi* (Pombe ikimwagika huwezi ukaichota yote). Wazo lililopo ni kuwa, janga likitokea halafu mali ikateketezwa, aliyepata hasara anastahili kwenda na kile kinachobakia. Kwa mfano, mfanyabiashara anaweza kupata ajali na bidhaa zake zikamwagika. Ni vile anavyovipata vikiwa vizuri ndivyo anavyoondoka navyo. Vingine vilivyoharibika vinaachwa pale.

*Uwukaana kamaya afuniaka inimbo* (Mtu asiyetaka vita huvunja fimbo yake). Kulingana na methali husika ni kwamba mtu akimshambulia mwenzake ambaye amevunja fimbo yake huwa mkosaji na anastahili kuadhibiwa na baraza la wazee. Katika jamii kuna watu wanaopenda vita na kuna wale ambao hawapendi. Wale wanaopenda vita huchokoza wenzao ili waanze kupigana. Kwa kawaida, wale wanaochokozwa na ambao hawataki kupigana huwa wanavunja fimbo zao. Mara nyingi jambo hili hutokea vijana wakiwa wamepeleka mifugo malishoni. Kuna wale wanaochochea wengine wapigane. Hivyo basi, wasiotaka kupigana huwa wanavunja fimbo zao. *Sheangakyi balekyela asi* (Kinachoruka angani, huwekewa mtego ardhini). Methali hii hutumiwa na wachawi wakimaanisha kuwa hata ukiwa mwangalifu kivipi, watakuroga. Yaani, watafanya liwezekanalo kuona kuwa wamekupata.

**6.2 Tahadhari**

*Nang'aulila akwa khumwanda kwentsofu* (Asiyeshika maonyo hufuata njia ya tembo). Ujumbe ni kuwa mtu anayepuuza maonyo hupatwa na hatari. Hii ni kwa sababu anaambiwa 'usifanye hivi na hasikii.' Mtu kama huyo mwishowe hupata tatizo.

*Indekhelo imali kane ikhukobose* (Sufuria nyeusi itakurudisha). Vilevile, kauli hii hutumika kwa ajili ya kutahadharisha watoto watukutu. Maana yake ni kuwa mtoto akimkaidi mamake na kwenda zake hurudi nyumbani wakati wa kula. Hivyo basi, kina mama hutumia methali hii kutahadharisha watoto wao walio watukutu.

*Umukyesi ebekama* (Mwerevu hajinyoi). Maneno haya pia hutumiwa katika kutahadharisha jamii husika. Lengo ni kufanya watu wajue kwamba mtu anastahili kushirikiana na wangine katika mambo mbalimbali (utangamano katika jamii). Kwani, kama ilivyo na kunyoa nywele, mtu hawezi akajifanyia kila jambo bila msaidizi. Ni lazima atahitaji usaidizi wakati fulani.

*Umukaaga abama na byosi* (Tajiri hawezi kuwa na kila kitu). Maana ni kuwa hata mtu akiwa tajiri kiasi gani, wakati mmoja atakosa kitu ambacho atamwomba mwenzake ambaye ni masikini. Kwa mtazamo huu, si vizuri tajiri kupuuza mtu masikini kwa sababu anaweza kumsaidia na kitu ambacho hana.

*Sheubweela imamo busilo* (Mzigo unaojifungia hauna uzito). Yaani, mtu anapofunga mzigo, anastahili kuweka kiasi ambacho anaweza kubeba. Akizidisha halafu ashindwe kubeba, hakuna anayemhurumia. Maana yake ni kuwa, mtu akizua mambo fulani, anastahili kuyatatua mwenyewe na akishindwa asiwalaumu wengine. Kwa hiyo, methali hii hu itumika kwa ajili ya kutahadharisha watu ili wafanye mambo kwa kuzingatia matokeo.

*Nambakha afila litwela* (Mtu anayejigamba huuawa kwa kuchomwa mkuki mmoja). Methali hii hutumiwa kutahadharisha watu wanaojigamba kuwa wapiganaji hodari. Maana hapa ni kwamba, haifai mtu kujigamba kabla ya vita kuanza. Kwani hajui linaloweza kutokea. Ni dhahiri kuwa mtu anayejigamba huwa wa kwanza kurushwa chini au pengine kuuawa na mpinzani wake.

*Kametsi kela uwakamanya* (Maji humuua mtu ambaye amezoea kuogelea). Tamko hili linamaanisha, hata kama mtu ana mazoea, anastahili kuwa mwangalifu katika mambo anayoyafanya. Asiyachukulie ovyoovyo akifikiria kuwa ana uzoevu. Yaani, tukio lolote baya linaweza kutokea kwake.

*Umwana ela uwasalakho* (Mtoto huua mwanamke aliyewahi kuzaa). Vilevile, methali hii inamaanisha kuwa, hata kama mtu ana mazoea, anastahili kuwa mwangalifu katika mambo anayoyafanya.

**6.3 Mafunzo**

*Isi walya naye lelo akhumemua imbo wa khumala* (Mtu uliyekula naye akikukwepa, jua tu kwamba amekumaliza). Hapa tunapata funzo kwamba mtu uliyekula naye mezani akianza kukukwepa, inaonesha kuwa amekwishachukua kila alichohitaji kukuroga na wakati wowote atakuua.

*Umuufi akanaama baamuba* (Mwizi hataki aibiwe). Hii ina maana kuwa mtu anayewafanyia wengine maovu, hataki afanyiwe mambo hayo. Anapofanyiwa, hulalamika sana. Methali hii hutumiwa kufunza watu kuwa wasifanyie wenzao mabaya.

*Ing'anda indwela inga yalulile khuntsu isululama* (Kifungu kimoja cha makuti kikidondoka kutoka kwenye paa la nyumba haiwezi kuvuja). Ujumbe hapa ni kuwa mtu mmoja akiondoka kwenye kundi la watu, kazi wanayoifanya haiwezi kukwama. Methali hii hutumiwa kuelimisha watu ambao wanatishia kuondoka kwenye makundi yao ya kikazi.

*Umwana akhupa eng'oma umukhulu washiina* (Mtoto anapiga ngoma mkubwa akacheza). Methali hii inafundisha kuwa, hata mtoto anaweza kumshauri mtu mzima. Maana ni kwamba si vizuri watu wazima kupuuza mawazo ya watoto kila wakati.

*Kukwo kwang'aba kubi ne kulayi* (Hata kama mtoto ni mbaya, kwa wazazi wake ni mzuri). Methali hii inaonesha mapenzi ya mzazi kwa mtoto wake. Hata kama mtoto ni mbaya, mzazi wake hataki kuona jambo baya linatokea kwake. Ingawa mtoto anaweza kukamatwa akiwa ameiba, mzazi hataki kumwona akiadhibiwa vikali.

*Umulebe utunda ne unyukhila* (Ukimrusha chini mtu wa ukoo wako katika mapigano, unampa nafasi ya kuinuka). Lengo kuu hapa ni kuonesha kuwa, si vizuri kuumiza jamaa yako. Kwani kwa mtu mwingine, unapiga kumjeruhi au kumuua lakini yule ambaye mna uhusiano wa kiukoo, unampiga kwa uzingativu ili usimuumize.

*Intsila yakama omulebe* (Njia hukoma kwa jamaa yako). Ufafanuzi wa maneno haya ni kuwa mtu huingia na kukaa kwa jamaa yake wala sio kwa yule ambaye hamjui. Kinachoelezwa ni kwamba mtu anaposafiri, huwa anapita nyumba nyingi za watu asiowajua na anapofika kwa ile ya jamaa, anaingia na kukaa. Anapofanya hivyo, anapaswa kuandaliwa chakula. Madhumuni ya methali hii ni kufunza watu wawe wawakaribishe jamaa zao.

*Ukhuwulile akhuupila iyowo* (Akushindaye nguvu anakupigia fimbo yako mwenyewe). Kulingana na methali hii, bila mtu kuwa na uhakika kwamba ana nguvu za kupigana, hastahili kuingia vitani. Hii ni kwa sababu, adui wake mwenye nguvu atampokonya fimbo na kumpigia. Kwa kuzingatia usemi huu, mtu akushindaye nguvu anaweza kukukuta umefanya kazi yako, akaiharibu na kuondoka kwa kiburi.

**6.4 Hekima**

*Umwana ekhalama khunebe* (Mtoto hakalii kiti). Lengo la kutumia maneno haya ni kufanya watoto wasichafue viti. Hii ni kwa sababu mtoto anaweza kwenda haja kubwa halafu bila kujipangusa anakalia kiti na kukichafua. Kwa hiyo, watu wazima huwa wanahekimisha watoto wao huku wakitumia methali husika. Kwa kufanya hivyo, watoto wanakua wakijua kuwa ni mwiko wao kukalia viti.

*Babana bekhalama khumayika* (Watu hawakalii mafiga). Wazazi wanatumia methali hii ili kulinda watoto wao wasiungue, jinsi wanavyoweza kukalia mafiga kama kuna moto wanaweza kuungua. Kwa kusema hivyo, watoto wanakua wakiwa na hofu ya kukalia mafiga.

*Babaana bekhalaama khushibwili* (Kinu hakikaliwi na watoto). Methali hii vilevile, inatumiwa kufanya watoto wasichafue vinu. Maana ya usemi huu ni kwamba mtoto ambaye amekwenda haja kubwa na hajajipangusa akikalia kinu anaweza kukichafua. Hivyo basi, kwa kuambiwa hivi, watoto wanakua huku wakijua kwamba ni tabia mbaya wao kukalia vinu.

**17.0 Mitindo katika Methali za Wamasaaba**

**1.7.1 Uteuzi wa Maneno**

Kwa kurejelea mifano ya methali ambazo zimetolewa hapo juu, tunaona kwamba methali za Wamasaaba huwa zinatumia maneno teule. Kama ilivyo na lugha zingine, Wamasaaba pia huteua maneno yanayostahili kutumiwa katika methali zao wakiwa na lengo la kuficha maana. Kwa mfano, *Umwana ela uwasalakho* (Mtoto huua mwanamke aliyewahi kuzaa). Hapa inabainika kuwa miongoni mwa maneno chungu nzima ya Kimasaaba, wao wanaamua kutumia maneno 'mwanamke, kuzaa na mtoto.' Hawajatumia maneno mengine kama vile mti, jiwe, panga kiti, n.k. Ni bayana kwamba mgeni akiisikia methali hii anaweza kufikiria wanazungumzia hali halisi ya kujifungua mtoto. Bali sivyo, wanazungumzia jambo tofauti kabisa. Maana iliyopo ni kuwa mtu mwenye uzoevu ndiye anaweza kushindwa bila kutarajia.

**7.2 Idadi ya Maneno**

Methali za Wamasaaba huwa na maneno machache sana. Huwa na maneno matatu, manne au matano. Ni methali chache sana ambazo huwa na maneno zaidi ya matano. Tukitazama mifano ambayo imetolewa, tunaona kuwa methali 27 kati ya 30 zina maneno matatu hadi manne. Methali mbili ndizo zina maneno 6. Methali moja tu ndiyo ina maneno 8. Hii inathibitisha kuwa methali ni sentensi fupi, kama wataalamu wengi wanavyosema.

**7.3 Matumizi ya Maneno ya Kawaida**

Kwa kuzingatia mifano ya methali ambazo zimetolewa hapo juu, tunaona kwamba methali za Wamasaaba zinatumia maneno ya kawaida ingawa yanahitaji hisia tambuzi ili kuelewa ujumbe. Mifano yote ya methali inathibitisha kuwa maneno ambayo yanatumiwa ni ya kawaida lakini huwa na ujumbe mzito ndani yao.Kwa mfano, *Shisili inga shafunikhile kumwini usomo kukundi* (Jembe likivunjika mpini, unatia mwingine). Katikamethali hii, maneno ambayo yametumiwa yanarejelea vitu halisi ambavyo ni jembe na mpini. Hata hivyo, ujumbe unaowasilishwa unahusiana na huzuni wazazi wanayoipata baada ya kumpoteza mtoto wao.

**7.4 Urejereaji wa Vitu vya Kawaida**

Methali za Wamasaaba kama ilivyo na zile za makabila mengine, hurejelea vitu vya kawaida. Tukitazama mifano ambayo imetolewa, tunaona kuwa methali zote 30 zinarejelea vitu vya kawaida. Yaani, vitu vyote ambavyo vimetajwa katika methali mbalimbali ni vitu vinavyopatikana katika jamii. Vitu kama vile jembe, mto, sufuria, ndoo, n.k.

**7.5 Matumizi ya Lugha ya Kisanaa**

Methali za Wamasaaba pia zinaonesha matumizi ya lugha ya kisanaa. Usanaa huu ndio unafanya methali kuwa na maana fiche. Bila kusuka lugha vizuri, methali haiwezi kuwa na maana fiche. Kwa mfano, *Bunuku bulyama lutwela* (Cheche za ngono haziji mara moja). Methali hii inaonesha jinsi wazungumzaji wanavyotumia lugha kisanaa ili kuonya watu wanaokuwa wakaidi baada ya kusaidiwa. Ni kweli kwamba katika jamii zetu kuna baadhi ya watu ambao baada ya kusaidiwa wanawatendea maovu wahisani wao. Kwa mfano, mtu anakopeshwa pesa na anakataa kulipa. Akidaiwa, anatumia matamshi ya kuudhi. Hivyo basi, Wamasaaba hutumia methali hii kuwaonya kuwa wakati utafika na watahitaji msaada tena.

**7.6 Matumizi ya Maelezo wala si Maswali**

Kwa kutazama mifano ya methali, inabainika wazi kuwa Wamasaaba huwa wanaendeleza methali zao kwa njia ya maelezo wala si maswali. Tukirejelea mifano ya methali ambayo imetolewa, tunaona kwamba methali zote 30 ni za kimaelezo. Hakuna methali zinazokaa kama maswali. Ni kweli kwamba kuna jamii zilizo na methali zinazokaa kama maswali, jambo ambalo halijajitokeza katika uchunguzi huu.

**7.7 Sauti ya Mzungumzaji**

Methali za Wamasaaba huwa zinatolewa kwa sauti ya wastani. Toni huwa si ya juu sana wala ya chini. Hata mzungumzaji akiwa amekasirika, sauti yake huwa

inashushwa kiasi wakati anapotumia methali kama onyo au tahadhari. Kwa mfano, *Nang'aulila akwa khumwanda kwe ntsofu*. Maana yake ni kwamba asiyekubali kushauriwa hushika njia ya tembo. Kwani wanamwambia asifuate njia husika kwa sababu anaweza kukutana na ndovu na anapuuza wale wanaomshauri na mwishowe anakutana naye na anamuua.

**7.8 Matumizi ya Sentensi Fupi**

Kama ilivyo katika lugha zingine, methali za Wamasaaba huwa ni sentensi fupi. Kwa mfano, badala ya kusema kuwa *Inga wandayo alikhusala baana nawe wakha khusala babowo* (Endapo ndugu yako ameanza kuzaa watoto, nawe unastahili kuanza kuzaa wako), wanasema tu kwamba '*Wandayo asala nawe usala'* (Ndugu yako anazaa nawe unazaa). Katika methali hii tunaona kwamba wazungumzaji wanaacha maneno hayo mengine ambayo yangefanya sentensi kuwa ndefu. Hii ni uthibitisho kuwa methali za Wamasaaba huwa fupi.

**7.9 Uwasilishaji wa Ujumbe wa Moja kwa Moja**

Ujumbe unaowasilishwa na methali hizi ni wa moja kwa moja. Hakuna kuzunguka na hakuna maelezo ya ziada. Maneno mawili au matatu yanatoa ujumbe kamili na unaoeleweka kwa msikilizaji. Kwa mfano, *Imumilo tsing'ayo emayo* (hakuna kucheza na koo). Maneno haya matatu yanatoa ujumbe wa moja kwa moja kwani ukikubali mtu acheze na koo anaweza kukuua.

**7.10 Miundo Inayoruhusu Watu wazima Kujibizana**

Wamasaaba ambao ni watu wazima wanaweza kujibizana kwa kutumia methali. Yaani, atolewaye methali anaweza kujibu kwa methali nyingine. Hii inaonesha ukomavu katika matumizi ya lugha. Kwa mfano, mzungumzaji anaweza kutumia methali kama hii kwa mwenzake; *Umushebi eshebama* (ngariba hajitahiri). Anayeambiwa methali hii anaweza kujibu kwa methali *Sheangakyi barekyela asi* (kinachoruka angani huwekewa mtego ardhini). Majibizano haya yanaonesha kuwa wazungumzaji hawa ni mahiri katika mambo ya uchawi. Yaani, wanachomaanisha ni kuwa mmoja akimfanyia mwenzake hiki, yeye atafanya kile.

**7.11 Miundo Isiyoruhusu Watoto Kujibu Methali**

Methali zinazoelekezwa kwa watoto huwa haziwaruhusu kujibu jinsi ilivyo kwamba ni tabia mbaya watoto kujibizana na wazazi au watu wazima. Pili, kauli zenyewe hutolewa kama onyo, tahadhari au funzo. Kwa hiyo, methali husika ikitumiwa, mtoto ambaye amekosea hatarajiwi kujibu. Kwa mfano, matumizi ya methali kama hii *Umwana ekhalama khuika* (mtoto hakalii figa). Methali hutolewa kama onyo kwa mtoto ambaye amekutwa akiwa amekaa kwenye figa. Hili ni funzo kwa watoto na hivyo hawatarajiwi kujibu. Methali hii inawasababisha

watoto kukua wakiwa na hofu kuwa ni kosa kwao kukaa kwenye mafiga. Lakini lengo ni kuwakinga ili wasije wakakaa kwenye mafiga kama kuna moto wakaungua.

**8.0 Hitimisho**

Kwa kuangalia methali ambazo zimechanganuliwa, inabainika wazi kuwa methali hizo hufuata mitindo maalumu. Mitindo hiyo ndiyo inasababaisha methali kupamba mazungumzo. Hali kadhalika, mitindo hufanya methali hizo kuwa na maana fiche. Kulingana na makala hii, lugha nyingi ambazo hazijakuzwa zina mambo mengi mazuri ya kifasihi. Lugha zenyewe zinaweza kuonekana kuwa duni lakini zina lundo la mambo ya kifasihi. Kwa hiyo, wanafasihi wana jukumu la kuzitafiti lugha mbalimbali za Kiafrika. Tunapendekeza utafiti mwingine ufanywe kuhusu vipengele vingine vya kifasihi kama vile tashbihi, istiara, shada na tanakali za sauti ili kukuza *Lumasaaba*. Tunapendekeza pia utafiti ufanywe kuhusu vipengele hivyo katika lugha za makabila tofautitofauti nchini Uganda ili kudhihirisha uzuri wa lugha hizo. Hali kadhalika, tunapendekeza utafiti kama huo ufanywe katika nchi za Afrika Mashariki na hata barani Afrika. Hii ni kwa sababu siku hizi watu wengi hawataki kujihusisha na lugha zao asili. Wengi wanaziona lugha zao kuwa ni duni. Kutokana na jambo hili, lugha nyingi za kiasili zimepoteza msamiati wake na zingine bado zinaendelea kuupoteza.

**Marejeleo**

Aleta, A.O. (2021). “Thematic Analysis of Oromo Proverbs Said about Women”. *International Journal for Innovation Education and Research.* 9: 561-573.

Bukenya, A., Gachanja, M. na Nandwa, J. (2008). *Introduction to Oral Literature*. Kampala: Phoenix publishers Limited.

Castagna, G. (2022). “A Collection of Jibbali/Śḥərɛ̄́t Proverbs from Ali al-Shahri’s Publication, The Language of Aad/عاد لغة, Old World”. *Journal of Ancient Africa and Eurasia*. 2:1-89.

Daniel, L. (2017). “What is the Definition of Language Style? Example of Socratic Q&A”. *Sage Journals.* 6:18-23.

Elunya J. (2009). Bamasaaba Abandon Lumasaaba for Luganda.” *ugandaradionetwork.net*,18:19.

Finnegan, R. (1977). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Gunawan F., Mayasari, R., Muna, W. and Masruddin, M. (2019). “Lecturers’ Language Style and Students’ Academic Self Efficacyin Higher Education of Indonesia”. *Arab World Journal (AWEJ).* 10: 77-87.

Indra, I. na Hamzah, H. (2018). "An Analysis of Language Style of Teenagers Found in Facebook Status". *E-Journal of English Language & Literature*. 7: 22-25.

Mbusya, M.C. na Chomba E. (2018). "Mielekeo ya Wanafunzi wa Kidato cha Tatu na cha Nne Kuhusu Methali Kinzani". *International Journal of Advanced Research* (*IJAR*). 6:1374-1381.

Mieder, W. (2016). "The Meaning of a Proverb: An American-Romanian Friendship in Paremiology". *Journal of the Western States Folklore Society*. 75:397-420.

Mulumba, P.M. (2021). "Some of our Languages are Slowly Dying out". Inapatikana katika www.monitor.co.ug. Imesomwa Julai 19, 2021.

Norrick, N.R. (2010). "The Meaning of a Proverb". *Journal of Language Teaching and Research.* 1:814.

Ogden, A.B. (2022). "Proverbs in Recent Research." *Sage Journals*. 20:131-132.

Omobola, O.C., Ajayi, H.O., na C.F. Olokunlade, C.F. (2014) "Pictorial Reading Strategy and the Learning of Proverbs and Riddles among Primary School Pupils." *International Journal of Innovation and Applied Studies.* 8: 1589-1593.

Reem A. (2022). "Processing Figurative Language: Evidence from Native and Non-native Speakers of English". *Journal of Frontiers Psychology*. 13: 1-5.

Samadi, N. (2022). "The Role of Proverbs and Textbooks in Teaching and Learning English Language." *Journal of Oscar Publishing Services.* 2:12-18.

Wamitila, K.W. (2003) *Fasihi Simulizi.* Nairobi: Muwa Publishers Limited.